**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SERENGETI SEKONDARI DAY.

**MEI, 2026**

**OFISI YA WAZIRI MKUU– TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**

**SHULE YA SEKONDARI SERENGETI DAY.**

**Namba za Simu**
**Mkuu wa Shule 0683325617**
**Makamu Mkuu wa Shule 0764248146**

**Shule ya Sekondari Serengeti day,**
**S.L.P 46, Mugumu-Serengeti.**

**Kumb: SDSS/Adm/Vol2/2026/13** **Tarehe 13/05/2026.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..........................................................................**
**S.L.P ……………**
**……………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SERENGETI SEKONDARI DAY HALMASHAURI YA SERENGETI MKOA MARA MWAKA.................**

## A. UTANGULIZI.

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari Serengeti day,ni **SHULE YA BWENI** na ipo umbali wa Kilometa **04** Kusini mwa Mji wa Mugumu Usafiri wa bodaboda kutoka mjini Mugumu serengeti unapatikana katika kituo cha mabasi Mugumu Nauli ni Shilingi **2000** kwa pikipiki.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe:**................** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **.............** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **..........................**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule ni Sketi ya kunguru yenye mchanganyiko wa rangi nyeupe,nyeusi na damu ya mzee (maruni) Unashauliwa uje ushonee sketi hizo shuleni ili kuepuka kukosea rangi na aina ya mshono.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Sare ya Michezo ni track suti ya rangi dark bluu.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu;
vii. Raba Nyeupe za michezo.
viii. Sweta mbili rangi Nyeusi
ix. Nguo za kushindia (*shamba dress*) mbili rangi ya kunguru angalizo,unashauliwa uje ushonee shuleni kuepuka changamoto ya mashono na rangi ya kimbaa kukosewa
x. Neck Tai mbili zenye kufanana na rangi ya sketi
xi. Tsheti ya shule yenye muhuri wa shule inapatikana shuleni kwa Tshs 12,000/= tu.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari **12** ya Quire mbili.
ii. **Ream mbili aina ya double (AA), tofauti na rimu tajwa haitapokelewa.**
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (HKL na HGL)
iv. Scientific Calculator kwa tahasusi ya HGL
v. Faili moja la kawaida la plastic la sh 2000 kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zako.
vi. Godoro jipya futi **2½** kwa **6**.
vii. Mashuka Jozi **2** (Blue na pink), blanket **1**, foronya ya godoro **1**, chandarua **1**.
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (**sahani, bakuli, kijiko na kikombe**);
x. **Ndoo 2** ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo kwa kuzingatia TAHASUSI

**HGL**- Kwanja **1**, Jembe **1**, Hardbloom1, Mopa 2 (ya kusukumia maji bafuni na ya nyunzi ya kudekia) Mifagio 2 wa ndani na nje aina ya chelewa,

**HKL-** Reki **1**, Mifagio **2** wa ndani na nje aina ya chelewa, Soft bloom**1**, Toilet brush**1**, Mopa **2 (**ya kusukumia maji bafuni na ya nyuzi ya kudekia)

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: MICHANGO YOTE ILIPWE KWENYE AKAUNTI YA SHULE NO: 3021200053 NMB JINA LA ACOUNT (SERENGETI SEKONDARY SCHOOL).**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni nanTaratibu utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha moja (1) ya kila mzazi na ndugu wa karibu wasiozidi wanne wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA SERENGETI**
**FOMU YA UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI**

**SEHEMU A: TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina la mwanafunzi ……………………………………………..kidato cha………...mwaka…..……

Shule ya msingi niliyosoma ……………………………iliyoko kata ya ……………………………

**SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI NA NDUGU**

i. Jina la Baba……………………………anaishi kijiji/mtaa……………………kata………………

Kazi yake……………………anuani yake ni……………………..…simu…………………………

ii. Jinala Mama……………………………anaishi kijiji/mtaa……………………kata………………..

Kazi yake……………………anuani yake ni………………………....simu……………………....

iii. Jina la ndugu……………………………anaishi kijiji/mtaa……………………kata…….…………

Kazi yake……………………anuani yake ni…………………….……simu……………..……….....

**C. TAMKO LA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO KWA WALIMU NA VIRANJA, UTORO, MAHUSIANO YA KIMAPENZI, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi………………………………………………………………………..(mwanafunzi), naahidi kuwa sitajihusisha/sitashiriki katika kupanga, kufanya wala kushabikia migomo kwa walimu na viranja, Utoro, mahusiano ya kimapenzi, fujo au makosa ya jinai nikiwa Serengeti sekondari katika muda wangu wa uanafunzi. Sahihi…………………………………………..tarehe…………………………………….

**SEHEMU D: TAMKO LA MZAZI/MLEZI**

Mimi ………………………………Mzazi/mlezi wa mwanafunzi………………………..…………

Nakiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo ya shule. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule ya Sekondari ya kutwa Serengeti katika kumlea mwanangu kwenye misingi bora na inayofaa.

Jina la mzazi/mlezi……………………………………............sahihi……………………………….

Tarehe…………………………………………………..Namba ya simu………………………….

**SERENGETI DAY SECONDARY SCHOOL**
**SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

TO THE MEDICAL OFFICER
…………………………………......
…………………………………….
Name of the Student……………………………………......................Form……………..……Year……………
Please, kindly examine the above named student to prove his/her fitness undertaking studies at our school.

1. X-ray……………………. 2. Urine……………… 3. Stool ……………………….
4. Physical fitness……………. 5. V.D ………………. 6.Tuberculosis ………………..

**A: PRELIMINARY INFORMATION (BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR)**

| | DISEASE | /NO | | DISEASE | YES/NO |
|---|---|---|---|---|---|
| | Tuberculosis | | | Epilepsy | |
| | Pneumonia | | | Ear, Nose and Throat | |
| | Asthma | | | Skin disorder disease | |
| | Heart trouble | | | Anemia | |
| | Recurrent indigestion | | | Operations | |
| | Jaundice | | | Serious accident | |
| | Kidney and Urinary trouble | | | Malaria | |
| | Dysentery | | | Stomach trouble | |
| | Nervous breakdown | | | Eye disorder | |

**B: VACCINATIONS AND INNOVULATIONS HISTORY**

| EASE | 1ST DATE | 2ND DATE | 3RD DATE |
|---|---|---|---|
| Small pox | | | |
| Whoop cough | | | |
| Measles | | | |
| Yellow fever | | | |
| Cholera | | | |

## C: MEDICAL EXAMINATION REPORT

a) Weight …………………………………………………………………………………….
b) Heart Beat …………………………………………………………………………….....
c) Vision etc ……………………………………………………………………………

## D: MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above, and consider that he/she is physically fit/unfit to undergo studies.
DOCTOR’S NAME ………………………………………SIGNATURE……..…………

DATE & OFFICIAL STAMP………………………………………………………………..

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI**

**UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0683325617.**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0764248146.**
- **Matron 0762407723.**

**KARIBUNI KATIKA SHULE HII**

**<u>A.C.M</u>**
**ANDREW C. MALELA.**
**MKUU WA SHULE.**

HEADMASTER
SERENGETI SECONDARY SCHOOL
P.O. BOX 46
MUGUMU – SERENGETI